# Maswali ya Vijana





# kwa Wazee

Wiki ya Wazee
9-14 May 2022

by Elimu Yetu Students

14/05/2022.

WIKI YA WAZEE.

WINNFRIDA. GODSON.

i/ Je ni kwanini zamani wasichana walikuwa-wanakeketwa na sasaivi hakuna hiyo kitu.

* ii) Kwanini wasichana wa zamani ikifika kipindi cha kukua (kuvunja ungo), walikuwa wanafungiwa ndani huku wakifundwa na wamama wakubwa, tofauti na sasaivi hilo swala limepotea. Je, ni sawa mila hiyo irudishwe sasa.

iii) Je, vyakula vya zamani vilikuwa vina nafasi gani mwilini tofauti na hivi vya kisasa.

14-05-2022

WIKI YA WAZEE

SABRINA SULAIMAN

- Je! Ni kweli au kunaukweli gani kwamba miaka ya zamani ilikua ni Lazima mwanamke azalie nyumbani na sio hospitali, alafu ndio aende hospital?

- Kwanini wazee wa zamani walikua wanapenda kupikia chakula chao kwenye kuni je ilikua ni mila kwao?

- Je! kwanini vijana wa zamani walikua wanatahiriwa Jandoni porini na vijana wasasa wanapelekwa hospitali tena wakiwa wadogo, Je! mila ya kutahiriwa jandoni na hospital ipi nzuri?

- Kwanini wazee wa zamani walikuwa wanapiga wake zao, tofauti na sasa.

- Kwanini vijana waliotahiriwa hospitali wanadha raulika tofauti na waliopelekwa jandoni,

kijiji chako (ulipozaliwa) kinaitwaje? Jina lina maana yeyote katika lugha yako?
Wazazi/babu/bibi waliishi wapi? Mababu yako wamekaa huko muda gani
Elezee
Dini ya asili ya kabila - wanaamini nini?
Je kuna hadithi ya mwanzo wa Kabila?
Rasilimali zipi zinapatikana Kijijini kwako?
Watu wangapi waliishi katika kijiji chako? Uliwafahamu wote? Leo maana asilia
* Mababu walifanya kazi gani? (Baba, Mama, Babu, baba yake...)
Makazi yako yalikuaje ulipokuwa mdogo? Yalitengenezaje?
Chanzo cha maji kilikuwa kipi? kukusanya maji kulikuwa kazi ya nani? kiasi gani kwa siku
watoto walipewa elimu na nani? Ya aina gani? Mlibebaje
* Mlicheza vipi ulipokuwa mdogo? (michezo ya asili) Wanyama wamebadilika?
Unakumbuka wanyama na mimea ya aina gani (taja jina kwa kilugha & kiswahili)
- Shabaha ya elimu ni nini?

- Orodheshe majina ya mababu yako (wengi unavyoweza)

- Tuambie hadithi aliyesimulia babu yako?

- Umeona Mabadiliko yapi katika 1) kijijini 2) Mjini 3) Nchini 4) Duniani

Unafikiriaje kuhusu dunia & nchi baada ya miaka 80. Itakuaje?

Vitabu vinavyohusiana

- Edible Wild Plants of Tanzania - Mimea ya pori yafaayo kula
www.maktaba.org/book/752

- Elimu ya kujitegemea
www.maktaba.org/book/1

- Mazingira Yako ya Kijiji - Your Village Environment
www.maktaba.org/book/569

Brighid McCarthy Brighid@elimuyetu.org

PRISCA MESHACK 14/05/2022

## WIKI YA WAZEE (MASWALI)

01. kwanini wazee wengi huwa hawapendi salamu na wanakuwa wa kwanza kuwasumbua vijana?

02. kwanini wazee wetu ndiyo wanakuwa wa kwanza kukimbia au kutofata mila na desturi zao wanaiga za kigeni?

03. Vyakula vya asili vingi huwa ni vizuri kwa afya zetu. lakini kila kitu chenye faida huwa na hasara, ni hasara gani za vyakula vya asili kwa mwili wabinadamu?

04. Ni kanuni gani au sheria nzuri zinazopaswa kufatwa katika famili ili watu wawe na maadili mazuri kwa vijana?

05.

AIKA - ELIREHEMA.

Swali 14/5/2022.

1 Ni kwanini zamani baadhi ya vyakula vilikuwa vina-katazwa kuliwa na Wanaume au Wanawake ila kwa-sasa havitiliwi Maanani kama enzi hizo?

2. Kwa sasa vijana hawa fati tamaduni, mila na desturi kama zamani ~~Ombi~~ kutokana na familia zinazo tulea ombi langu Mkazie Mkazo kwa vijana yale yaliyokuwa yanaleta heshima zamani ili yazidi kudumishwa kwaupya kama vile kurejesha heshima ya Mavazi, Mikao mizuri kwa vijana. ili ku ondoa aibu zinazopelekea wazazi au-wazee wetu kutukanwa (kuchafuliwa) kutokana na vijana-kuiga Mila tofauti [za kigeni]

Maswali Kutoka kwa wazee...... 14·05·2022
Mwaka 2022 Siku ya Jumamosi

CATHBERT CHARLES

1 Nikwanini zamani walikuwa mama walikuwa wanajifungulia njumbani?
2 Nikwanini Zamani Kulikuwa na Mambo ya Uganga Uganga?
3 Kwanini Zamani wazee wetu walikuwa Wanawakeketa Dada zetu?
4 Kwanini Babu zetu na Bibi zetu walikuwa wanawaozesha Dada zetu Kama ni mweupe mwanaume anatoa ngombe nyingi?
5. Kwanini wazee wasasahivi ~~kama~~ wanakuja mapema?
6. Nikwanini Vijijini hamna magonjwa ya Zaman?
7. Kwanini Kulikuwa na mizimu?

MASWALI ~~YA~~ KWA WAZEE 14·5·2022

ELIA ASHERI

1) Kwanin ulikuwa na utamaduni
2) Je nin utamaduni ni etuchawi kama mila
3) Kwanin sisi vijana ~~hatuki~~ ~~huta~~ huubali utamaduni
4) Kwann mziki sasa na yazamani ~~z~~ tofauti

~~[illegible]~~

PASCAL BENSON 14/5/2022

VIKAO YA WAZEE

1. Kwanini zamani Mwanaume ana chaguliwa Mwanamke wa kuoa na Mwanamke ana chaguliwa wanaume wa kumuoa.

SALOME DAUD

WIKI KWA ~~KAZEE~~ WAZEE

~~Kwa nini Kuna Vyakula Vya Asli~~

Kwanini kuna vyakula vya asili?

Brightness Manase

WIKI YA WAZEE & 14 May 2022

1. kwanini wazee zamani walipenda kutembeleana wao kwa wao.

2. kwanini laana ya mama inakuwa/inaishi lakini baba haiishi.

3. kwanini wasichana wa zamani walikuwa wanatekwa na ni kweli walikuwa wanapoteza hamu ya mapenzi.

JANETH ABISIAS NKALIKUMBA 14/5/2022

# WIKI YA WAZEE!

Q1: Kwanini wazee wa zamani walikuwa wanapenda sana kuamini mila potofu na haswa walikuwa wakipenda kuabudu Miungu mfano Mti, n.k.

Q2: Kwanini wanawake wa zamani walikuwa wakibaguliwa wakati wa chakula walikuwa hawatakiwi kula na wazee pamoja mpaka wao washibe ndo wanawake wakala chakula.

NAPENDA AHAB SIMON.

14/5/2022

# WIKI YA WAZEE

MASWALI;

01! Kwa nini wanawake wa Makabila tofauti tofauti wakisalimia wanashuka chini kidogo au wengine wanapiga magoti kabisa. Hivyo hamuoni kwamba hiyo ni unyanyasaji wa kijinsia kwa sababu kwa upande wa wanaume wao wanasimama kawaida?

02! Kuhusu swala la Mila na desturi ambazo zilikuwa za zamani kama ndoa za utotoni, ukeketaji, na kumpiga mwanamke. Labda hizi mila tukiendeleza na hizo mila zitatuletea madhara.

JOHN PATRICK

14/may/2022

WIKI YA WAZEE

1) Kwanini wazee wa kimasai walikuwa wanaoa wanawake wengi Je? Ina umuhimu gani

2) Wazee wazamani walikuwa wanaabudu miti na milima Pia walikuwa wanapata mafaniko mfano, mvua—— Je? imani yao ilikuwa ina msaramo gani au ilikuwa Ipoje?

LULU-JUSTINE.

1. Kwanini vyakula vya kizamani ni tofauti na vyakula vya sasa?

2. Kwanini tamaduni za kimasai wanapotoa amri wauelana wataiiriwe wengine wakakiuka amri hiyo na kwenda kuwatairi watoto wao maospitalini kwanini wanachukuliwa hatua kali?

3. Kwanini watu wa zamani walikuwa wanavaa nguo za heshima kuliko hawa wa sasa hivi?

4. Ni kweli kuwa kila tamaduni inafata amri na mila zao?

5. Kwanini watu wa zamani wanatumia dawa za asili wakati wakiamini ndo zinatibu kuliko za sasa?

6. Kwanini utandawazi umeletwa kwa faida na hasara? na kama ni kwa faida na hasara fafanua?

7. Kwanini wanawake wa zamani wakiwa na bikra wanadhaminiwa zaidi / kuliko ambao hawana.

8. Kwanini wazazi wa zamani walikua wanachagulia watoto wao wanaume?

9. Kwanini Mila ya kimasai / Wazazi wa kimasai wanawaoze sha watoto wao wakiwa tumboni

10. Kwanini wazee / Mila za zamani zilikuwa zik abudu mfungu tofauti?

11. Kwanini Wamasai / Mila za kimasai wanapoanza

Zulu-Justine.

1. Kwanini vyakula vya kizamani ni tofauti na vyakula vya sasa?

2. Kwanini tamaduni za kimasai wanapotoa amri wavulana watairiwe wengine wakakiuka amri hiyo na kwenda kuwatairi watoto wao maospitalini kwanini wanachukuliwa hatua kali?

3. Kwanini watu wa zamani walikuwa wanavaa nguo za heshima kuliko hawa wa sasa hivi?

4. Ni kweli kuwa kila tamaduni inafata Amri na mila zao?

5. Kwanini watu wa zamani wanatumia dawa za asili wakati wakiamini ndo zinatibu kuliko za sasa?

6. Kwanini utandawazi umeletwa kwa faida na hasara? Na kama ni kwa faida na hasara fafanua?

7. Kwanini wanawake wa zamani wakiwa na bikra wanadhaminiwa zaidi / kuliko ambao hawana.

8. Kwanini wazazi wa zamani walikuwa wanachagulia watoto wao wanaume?

9. Kwanini Mila ya kimasai / Wazazi wa kimasai wanawaoze sha watoto wao wakiwa tumboni?

10. Kwanini wazee / Mila za zamani zilikuwa zik abudu mizungu tofauti?

11. Kwanini Wamasai / Mila za kimasai wanapoanza

Kwataini watoto wa kiume wanakuwa na msamu Mfano wanakuwa na jibu ambalo walikuwa mualiza kwataini vijana wa wanawake mitaani kumwagika maisha na baadaye ya kupa wanafunga jibu hilo na ama kwataini vijana mpaka mda mwingine upite kwanini janani?

Wiki ya wazee

JACKLINE PETER

* Kwanini zamani kulikuwa na mila na tamaduni mbali mbali na ilikuwa ni lazima zifuatwe. .

* pia kwanini kila tamaduni inakuwa desturi tofauti tofauti

WIKI YA WAZEE SIKU YA JUMAMOSI 14 May 2022

MAKALA MUSSA

Kwanini Kutukuwa na Majambazi Sugu hawakamatiki Nawakikamatoka wakawa Selo kuwa wengine wanagenka njooka?

Uchawi Umeanzaje Asaje

ELIMU YETU ORGANIZATION

SIKU YA WAZEE

14/05/2020

DAVID . KIMAY

MASWALI:

1. Je ni tabia zipi au ni mienendo ipi enzi zenu. ilikuwa inapigwa vita sana na wazazi wenu. pindi nyie mkiwa vijana kama sisi

2. Je ni Sababu gani Zinawafanya Vijana Kukiuka. kuishi vile au yale wanayofundishwa na wazee au wazazi. wao.

3. Je ni kipi kifanyike ili kusaidia vijana wanao haribika kwa sababu ya utandawazi?

## WIKI YA WAZEE

14/05/2022

## KIKAO CHA WAZEE NA VIJANA

## MASWALI KWA WAZEE

## FLORIANI-FERDINAND

∴ SWALI

1: Zamani wazazi inasemekana kwamba wazazi walikuwa hawakubali kuendelea kuishi na kijana aliye fikiesha umri wa kuwa kijana au kujitegemea walikuwa wanafukuzwa nyumbani wakaanzishe maisha yao. Je ina athari gani kwa wazazi wa sasa hivi wanaoendelea kuishi na vijana ambao wamefikisha umri wa kujitegemea?

14/5/2022
—*—*—

HAPPY * DAUDI

i) Kama vijana hawata elewa namna wanavyoeleweshwa kuhusu tamaduni zao wazee watatumia mbinu gani mbadala ili kuhakikisha vijana wataelimika kwa kiwango kikubwa.

ii) Kwanini enzi za Zamani walikuwa wakiamini kuwa mwanamke hawezi kuwa kiongozi ?

PRISCA - LUCAS.        14/5/2022.

1: Kwanini Enzi za zamani wazee waliamini ukeketaji wa wanawake inawasaidia kuondokana na magonjwa Lakini kwa sasa wanamini kuwa ni unyanyasaji wa kijinsia.

2: Kwanini zamani wanawake walikuwa wanaolewa wakiwa na umri mdogo na mwanaume aliyemzidi umri. na sasa kizazi au taifa kiujumla kinapiga vita ilo suala.

WINNIE FRANCIS

14/5/2022

## MASWALI KWA WAZEE WETU

1. Samahani naomba kuuliza swali

Ni kwanini wazee ukiwasalimia hawaitiki atakwambia "Mambo", Kwema au wengine wanakuambia "Unaminyima nini" Sasa hapo mnatushaurije sisi kama vijana wenu

WIKI YA WAZEE 14.5.2022.

* Miziki ya sasa na ya zamani hina utofauti mkubwa sana lakini kwa sasa vijana wengi wanajali miziki ya ~~sasa~~ sasa kuliko miziki ya zamani wanaona kama haina maana Hivo una washauri vijana wa thamini sana miziki ya zamani maana inabeba ujumbe na maana?

* Vijana wengi wanakuwa wana Huwa tabia mbaya nammonyoko wa maadili kwa wazee na kuto kuwaheshimu kabisa Hivo uta washauri nini Vijana wawe namaadili mema kwa wazee?

* Ni vyakula gani ambavyo mnaweza kutushauri sisi kama vijana kutumia navinaweza kuimarisha na kuboresha miili yetu?

EHWAZA Josia

## WIKI YA WAZEE JUMAMOSI.

PETER SOSPETER : Tar, 14-05-022.

1. ~~Kip~~ Maswali.

- Kipindi cha zamani wanawake walikuwa chini ya uongozi wa wanaume, kabika uongozi, elimu, pia na kazi. Lakini kipindi cha utandawazi zimekuja sheria za usawa wa jinsia.
  - Je, ni vizuri usawa kati ya mwanaume na mwanamke.

- Miaka ya zamani vita na vitendo viovu vilikuwepo kwa kasi sana mf; unyanyasaji, vita, vifo na rushwa.
  Je ni kwanini vita na vyote viovu vilikuwepo na sio miaka ya utandawazi

AMANI KIBALI.                                                  14·05·2022

* Wazee wetu wanatushauri nini kuhusu sisi vijana kudumisha mila na desturi zetu kwa kipindi hiki?
* Je wazee walikuwa wanapenda kuimba na kucheza ngoma wakati gani sana sana. na ni kwa nini?

VANESSA EMMANUEL KILEO.

WIKI YA WAZEE

1. Je Kuna umuhimu gani wa vijana wa sasa Kufata tamaduni za zamani?

ELISHA YOHANA TIERE 14/5/2022

WIKI YA WAZEE

Maswali:

1: Ni kwa nini baadhi ya makabila Tanzania wana mila na desturi za kukeketa watoto au Tohara ingalikuwa wanajua yakuwa ina madhara?

2. Ni kwanini wanaume wa kimasai wanaowaachia wanawake majukumu yote ya kifamilia

3. Ina maana gani wanaume wa kimasai kutoboa au kuchana maskio yao?

4. Baadhi ya vyakula vya asili mfano supu, huchanganywa na damu mbichi?

5. Ni kwanini wanaume wa kimasai wanatabia ya kuposa binti ingalikuwa ni mdogo?

6. Kuna umuhimu gani wa kuchaguliwa binti au kijana wa kuoa?

EZEKIEL LAIZER

# ELIMU YETU DEVELOPMENT ORGANIZATIO

14/05/2022: KIKAO CHA WAZEE.

1. Ni Kwanini Mila na desturi za Makabila kwa Mfano kabila la kimasai huwa wanakuwa na Matam bilco Mengi, hivyo basi kuweza kusababisha Migogoro ya kifamilia au jamii kwa ujumla.

2. Kwanini baadhi ya Makabila huwa hawawapi wan awake kipaumbele kweye elimu

JULIANA ROMAN. 14/05/2022

1) Ni kwanini wanawake wa Zamani walikua wanajiheshimu sana kuanzia kwenye mavazi mpaka nidhamu. na ni kivipi walikua wanakubalika sana na Jamii ?

2). Ni kwanini wazazi wetu wa kisasa wanaenda na utandawazi Atupati Vile vyakula vya asili tupanjaje ili kuwapanga wazazi wetu kutuandalia vile vyakula vya asili ili tuweze kupata nguvu na afya kama Wazee wa zamani ?

3). Kwanini Wazee wa zamani walikua wakitumia dawa za kienyeji na zilikua zikiwasaidia kwa kiasi gani ?

4). Na kunatofauti gani kati ya dawa za kienyeji na za kisasa ?

5). Ni kwanini baadhi ya makabila walikua wanabaguana kwenye vyakula mfano. Wamasai awali wanaume kitalolok

6). Kwanini zamani kulikua kuna maswala ya ukeketaji na Je ni kwanini ?

7). Je ni kwanini Wazee wa zamani walikua wanaabudu Sana kwenye miti, mawe, mito, na mifugo ?

8). Ni kwanini kukitokea ukame wazee wa zamani walikua wanaweza kuita mvua ?

ASHRAPH ADRIAN

WIKI YA WAZEE

14/05/2022

* Je unahisi ndani ya miaka 20 ya baadae mila na desturi zetu zitakuwa bado zinafanyiwa kazi?

* Kwa nini vyakula vya asili huwa vinaliwa tu wakati tukiwa vijijini lakini sio mjini?

* Kwa nini wazee wa zamani walikuwa hawana uhuru wa kuongea ama kujielezea kama vijana na watoto wa kizazi hiki cha sasa? *

14/05/2022

# WIKI YA WAZEE.

*MOUREEN NICHOLAUS.

> Je, zamani ilikuwa kuna tabia ya kuzaa na mwanamke kwanza kabla ya kumuoa kwa kigezo cha kupima kama ana uzao? Kwa maana kwa miaka ya sasahivi vijana wengi huwa wanahitaji kwanza kuzaa na huyo mwanamke alafu ndo amuoe kwani wana msemo usemao kuwa hawahitaji kuuziwa mbuzi kwenye gunia?!

*> Zamani kulikuwa na mila ya kwamba wazee wakichinja wanawapa wanawake mautumbo na mawashi washi huku wao wakibaki na zile nyama nzuri nzuri kama steki, maini, kidari na vinginevyo vile vinono. Je hiyo ni mila nzuri?

*> Kwanini wazee wa zamani walikuwa hawalali pamoja na wake zao bali wanawake ndo walikuwa wanalala na watoto na syo ~~wam~~ waume zao. Je hiyo ni sahihi?

> Mbona zamani kulikuwa hamna matukio mengi ya ubakaji tofauti na sasa?

> Kwa sasa wazee wengi waume kwa wake wanapenda watoto wadogo wadogo wawenao kimahusiano. Je, hiyo ni sawa na mwanzo?

> Kwanini wazee wa zamani walikuwa wakianza kula kwanza wao alafu wakishiba na wakirithika ndo watoto na mama ndo wanafuata. Je, mida hiyo ni sahihi kuifuata

JORDAN JOSEPH

1) Je mila na desturi za zamani ni Sahihi kwa Sisi vijana kuzipata kwani kuna. Baadhi ya mila hizo zimepitwa na wakati

2.) Je kati ya mila, desturi na dini kipi kina mamlaka juu ya kingine kwani kuna - Baadhi ya mila zinakosolewa na dini

3.) Kwanini Utaratibu wa kuoa kwa kila kabila unaubana Sana Upande wa mwanaume

4) Je ni haki kulipa mahari na inamaana gani katika familia au jamii na nani anafaidika na hiyo mahari

5) Je tufanye nini ili kuwaenzi wazee wetu?

6) Je mliwezaje kuishi na wake zenu kwa kupitia kilimo tu

Collins Moses

Jumamosi

# WIKI YA WAZEE

14.05.2022

I. Wazee wetu je! na nyinyi mlipewa njia za kuishi katika mienendo bora katika jamii?

Juneth Kirunyo

1. Kwanini kabilala kimasai wanaume wana tairiwa wakiwa wakubwa na sio wadogo kwani wakitairiwa wakiwa wadogo ina madhara gani?

KELVIN INOCENT SIKU YA WAZEE 14.05.2022

1. Kuna pombe za asili ambazo tumezaliwa tukazikuta (mbege, mzo...
a) na zinalewesha ni vizuri sisi vijana kuzitumia au vipi

ANGELUS DEOGRATIUS ; WIKI YA WAZEE 9-14/05/2022.

1. Mila na desturi zetu zina umuhimu kwetu na faida zake pia, na hatupaswi kuziacha. Je vipi kuhusu zile mila na desturi kama, (ukeketaji, ndoa za utotoni na kurithiana wake?)...

2: Je kuna umuhimu wowote wa kuendelea kutumia njia za zamani au njia zilizokuwa zikitumika zamani kama vyanzo vya usafiri wakati njia za kisasa zipo??

3: Je wazee au wahenga wana umuhimu wa kubadilika na kuishi kisasa kama dunia ya sasa ilivyo..

WIKI YA WAZEE 14/5/2022

IVON - CHRISTOPHER

1. Je ni kifanyike kumshauri au kumfanya kijana/vijana wa sasa kua na maadili kama ya vijana wa zama

2. utamshauri vipi vijana wa sasa kula vyakula vya asili

* 3. Je ni nini kifanyike kurudisha Utamaduni na mila za zamani kwa vijana wa sasa

4.

Ally A Ally
14/5/2022

1) Vijana wa Sasa wengi wamezaliwa mjini na wengi wetu hatujui Mila na desturi zetu. Je nyinyi kama wazee mutafanyaje ili mila desturi zetu zisipotee? *

2) Mila na desturi kama ukeketaji na kuto kula baadhi ya vyakula ziki tokewa kutakuwa kuna kiuka??

KICH ~~ALEX~~ 9-14/5/2022.

WIKI YA WAZEE

1. Je, ni kwanini inasemekana vyakula vya asili ni bora kuliko vyakula vya kisasa kwa afya bora.

JUMAMOSI
TAR: 14/05/022

CHRISS - DIOMEDY

# WIKI YA WAZEE

Swali: Kutokana na mila na tamaduni za wazee wetu wa zamani ilikuwa uwezi kuoa wal[illegible] kuolewa pasipo kuchaguliwa mume au mke na wazee tunaoishi nao. Je, ni Sababu zipi zilizopelekea mila ya kuchaguliwa mchumba kutoweka katika kizazi cha sasa ambacho Sasahivi uwezi kuchaguliwa mke au mum[illegible] na wazee wetu kama hapo mwanzo?

ELIMU YETU: DEVELOPMENT ORGANAIZATION"

14:5:2022 / MIKE JUNIOR.

① No 01 * Kwanini wasukuma wakienda shambani huwa na ushirikiano na huwa wana bebana wengi karbia nusu ya kijiji wanaenda kulima shamba moja na kuimba nyimbo za maadili na za kitamaduni.

TUNU RAMADHANI

*1: Je vijana wanapaswa kufuata utandawazi ? au kuendelea na mila za zamani ? na kama ni ndio hizo mila zitawasaidia nini kuendana na teknolojia ya sasa.

2: Je nikweli kwamba unyago kwa wasichana ulikuwa ukisababisha mimba na ndoa za utotoni ndiyo maana kwa sasa zimepuuzwa ili kuepusha mimba hizo pamoja na ndoa za utotoni ?

IVANY. 14.05.2022.

1. Kwanini tunapinga Utamaduni na desturi za Makabila ambayo yanafanya Ukekelaji wakati ni Mila na desturi Zao?

2. Wazee wa Zamani walikuwa wanatumia vitu kama tumbaku, Ugoro, pombe za kiasili hiyo ilikuwa Utamaduni na desturi zao Kwanini hivi Sasa Serikali inapiga vita wakati ni mila na desturi zet

3. Ukiangalia Zamani na Sasa kuna ut ofauti mkubwa Sana, kuoa au kuolewa ilikuwa makabila kwa makabila, mfano mmasai kwa Mmasai ila hakukua na maendeleo lakini Karne hii mnaoana mchaga kwa Mmasai mkiunganisha Makabila hayo basi maendeleo yato kuwepo kwahiyo hauoni kwamba Zamani kulikuwa na maendeleo mabaya Kuliko Sahivi?

JOYCE xxxx LAIS

14.5.2022

WIKI YA WAZEE:

01. Kwanini vyakula vya kizamani zina nguvu kuliko vyakula vya sasa.

02. Vyakula vya kizamani na vyakula vya sasa zipi zinajenga mwili.

Fabian Julius 14/05/2021

Wiki ya wazee

- Wazee mnaweza kutuelekeza namna yakutembea

3. Je wazee wetu njia zipi au ni mbinu zipi mlitumia kuishi na kufata mila na tamaduni zetu ?

WIKI YA WAZEE 14/5/2022 JUMAMOSI

LOTHY LUCUMAY

1 Wazee ~~At~~ mliwezaje kuishi na wake zenu/mabwana wenu kwa mda mrefu tofauti na vijana kwa sasahi ?

2 Je Nyie wazee mliwezaje kuepukana na maradhi yaani kuto kupata magonjwa mbali mbali kila mara tofauti na vijana wa sasa, Kwasababu vijana hawa wanaonekana kupata maradhi ya kila aina kwa haraka zaidi ?

# NASRA HALFA HASSAN

## WIKI YA WAZEE

## MASWALI

14:05:2022

1. Je kuna umuhimu gani kwa vijana kufata mila na desturi za zamani kuliko kuripuuza na kufata utamaduni wa watu wengine.

2. Je ~~vya~~ vyakula vya Asili vina umuhimu gani au vina Faida gani kwa vijana na wazee.

GLORY M'BONDEI

Te 14th May 2022

1. Kwanini watu wa zamani walikuwa wanapenda kufanya Matambiko kuliko kuamwamini Mungu.

2. Watu au wazee walikuwa wanazaa watoto wengi kuliko sasaivi Ni kwanini

~~OLTESH · N. LAIZER~~

OLTESH · N. LAIZER

WIKI YA WAZEE

1. Ni ~~dawa~~ kitu gani kijana wa zamani ali kwa ana takiwa kufanya?

2.

JENIPHA BRANSON 14/5/2022.

Dawa ya asili ya majipu ni nini?

kwanini wasichana wa kimasai wanaolewa wakiwa na umri mdogo?.

Dawa ya asili ya tumbo ni nini.

14/5/2022.

VAILETH-MEDSON

1. Ni kwanini wasichana wa zamani walikua wanafanyiwa tohara

2. Ni kwanini Ndoa za zamani zilikua zinadumu kuliko Saivi

DERICK BONIFACE SINDE 14/5/2021

MASWALI:

1: Je ni njia zipi zilikuwa zikitumika na wazee wazamani kulinda wanawake na matendo ya unyanyasaji wa kijinsia dhidi ya ~~wanawake~~ wanaume

2:

EMMY GASĪO

* Ni kwanini ndoa za ~~zamani~~ sasaivi azidumu kama za zamani

Na ni njia gani zutatumia kwa sisi tunao enda kuingia kwa ndoa ili tujiokoe kwenye janga ili?

ELIYA AMINIEL 14 May 2022

WIKII YA WAZEE

- Je Vijana wa sasa twende na utandawazi au tuache?

•

14th May 2022. WIKI YA WAZEE.

SIKU YA JUMAMOSI.

1. Kwanini vijana wa sasa hawafuati mila na desturi kama zamani wazee walivyokua wanafanya?
2. Kwanini vijana wa sasa hawali vyakula vya asili tofauti na wazee wetu wa zamani?

14/05/2022

WIKI YA WAZEE

ESTHE ATALYNS

* JE Kwanini mabinti wa zamani wakiolewa wakigombana na waume zao wakirudi kwa wazazi hawapokelewi?
* Kwanini mila na desturi za zamani haziendelei?
* Kwanini wanawake wa zamani wanazalia nyumbani hawapati matatizo yoyote na watoto hawapati chanjo yoyote na wanakuwa vizuri?

14/05/2022

WIKI YA WAZEE

ABASI HAMISI ABASI

(i) Kwanini Zamani makabila mengi huwa wanachagua gwa mwanamke wa kuowa.

(ii) Kwanini ukeketaji kwa wanawuke umekatazwa kwa sasa na Zamani ilikuwa na Tamaduni

Janeth Kiwazo

14/05/2022

WIKI YA WAZEE

1: Njia gani zilitumika kuzuia utandawazi enzi za zamani?

14/May/2022

# WIKI YA WAZEE

## Swali

i) kwanini kipindi cha zamani wazee wengi walikuwa wanaamini mizimu badala ya nguvu na juhudi zao wenyewe

By collins Nicolas

MARTIN MOSSES 14/05/2022

1Y Ni changamoto gani huwa mnapitia kutokea kwa vijana wanao wazunguka.

2Y Kutokana na mila na desturi zetu wazee wa Zamani walikuwa wanavaa ngozi ambazo walikuwa wanaficha sehemu za siri na kiunoni kwa — wanawake je kutokana na mila pia tunatakiwa kuvaa hayo mavazi ingalikuwa ~~k~~ kwa sasa ni teknolojia.

14/5/2022 WIKI YA WAZEE MICHAEL ELIAS

01 Kwani Siku /Miaka ya Zamani: Mtu alikua anachaguliwa Mke so Yeye anachagua atakama Awe Ajampenda.

EVAREST FRANCE MLAY 14/5/2022

1 Kwanini mila na desturi za kimasai mtoto wa kike analipiwa mahari akiwa tumboni ~~huoni~~ huoni ni kukatisha malengo yake alezaliwa?

2. kuanini mila na desturi zilikuwa zinaruhusu kuchaguliwa mke ata ambaye hujampenda?

ESTER MASUNGA.

14th May 2022

## WIKI YA WAZEE

1. Kwanini mila na desturi za wamasai zinaruhusu wanawake kufanya kazi, kulisha familia alafu waume zao wakiwa nyumbani wakisubiri kuletewa

14·5·2022

GERALD JONS.

WIKI YA WAZEE

1. Sina Swali ila nawashukuru Wazee wetu kwa kutenga mda wao kwa ajili ya kutu.elimisha vijana

WIKI YA WAZEE 14·05·2022

ANGEL MATHEW

MASWALI

1: Ni Kwanini Vijana wa sasa awana nidhamu ~~sa~~ Kama vijana wa ~~th~~ Zamani na ni mbinu gani zinaweza Kutu miko Kuwafanya wawe Kama wa ~~d~~ Zamani

2: Ni Kwanini Ndoa za Sasa Si Sawa na ndoa za — — zamani:

3 Je Kipindi cha Zamani Wazee ~~za~~ wetu walitumia nini Kujua Mda pia walitumia mbinu gani

4 Je ni madharo ~~ya~~ gani Kijana atapata pindi atakapo Kuo anapofundishwa maadili mema na Kuyapotezaa. Pia Ushauri wenu wazee wetu ni upi.

5: Je mtu mwenye nidhamu utamtambua Kwa mavazi tuu

USHAURI / MAPENDEKEZO

Mimi Kama mimi ningependa wazee wetu Muwe mna tenga ~~Siku~~ Angalau Siku moja Kwenye Wiki moja mzidi Kutufundisha maana tunashauku zaidi yakutambua Kuhusu Mambo yaliyopita.

# WIKI YA WAZEE

GRACE CHARLES 14/5/2022

1. Mila na desturi zenu zilikuwa mtu akifanya kosa anaadhibiwa na mtu yeyote kwenye familia au kwenye jamii je, Amekwenda kwenye tamaduni zingine akafanya kosa hiyo jamii aliyoenda wanaweza kuadhibiwa ipasavyo?

2. Hivyo vyakula vyenu vya asili vilikuwa vinaliwa mpaka kwenye sherehe au tafrija yoyote kwenye jamii au sehemu hiyo?

3. Je, Hizo kaniki mlikuwa mnapata wapi wakati kulikuwa Hakuna viwanda vingi?
Au ni serikali ilikuwa inawaletea kiffffni?

SELEMANI ALLY 14/5/2022

(Kisicho)

Maswali:

1. Kwanini Wanaume wa kimasai hawaruhusiwi kula kitalolo?

2. Kwanini watoto wa kimasai wakiwa machungani kuchung ngombe vibobo wakati wakubwa wao wa- wanawekewa chakula kwenye nagewa pesa?

14.05.2022

ZULFA HAMADI

- Je ni kwa nini mila na desturi zetu kipindi cha nyuma muda wa kula wazee wanakaa upande wao hawashirikiani na wanawake au wakinamama?

- Ni kwa nini mila ya kimasai watoto wakike hawaruhusiwi kwenda machunganii. Ni wa kiume tu?

- Je ni kwa nini mila na desturi za wachaga wanapenda kupeleka kinywaji kama vile mbege makaburini?

14-05 May 2022 Junior -Daotan

WIKI YA WAZEE

B) Maswali

1 1) Ni kwa nini Vijana wasasa hawapendi kudumisha mila na desturi zao za zamani

2) Ni kwa nini Vijana wengi hawapendi kuwa Wazazi ya heshima

3) Vijana Je ni kwa nini Vijana wasasa hawapendi kujua mila na Vyakula vya kiutamaduni

4) Vijana wasasa ni kwa nini hawapendi kujua michezo ya wazee wa Zamani ambao waliyo kuwa wakicheza mfano bao na kukimbia kwenye gunia

JOYCE GASPER.

1: Kuna mila na desturi za zamani kamavile ndoa za mitara ambazo haziruhusiwi. katika jamii Je mavazi mliyokuwa mnavaa ni sahihi kulingana na muda huu?

2. Je nikosa la vijana kuvaa mavazi wanayoyavaa kwa sasa au ni kutokana na teknolojia waliyoikuta kwa wazazi?

WIKI YA WAZEE 14/5/2022

AMELINA FRANK

1. Je nini kifanyike kurudisha Tamaduni na mila za zamani kwa jamii ya sasa???

2. Kifanyike nini kumfanya kijana wa zamani na wasasa - wafanane mila na desturi za zamani kwani vijana wengi wa sasa wamejikita sana kwenye utandawazi???

3. Utamshauri vipi kijana / vijana wa sasa kula vile vyakula vya asili kwani vizazi vya sasa vimejikita sana kwenye vyakula vya kisasa kuliko vya zamani

HAPPY RICHARD 14/5/2022

WIKI YA WAZEE

1. Hivi vijana wasipozingatia mila na desturi za zamani watapata madhara gani

2. Nini kifanyike ili vijana wa sasa hivi wazidi kudumisha mila na desturi zetu za zamani

14th MAY 022

ELINE JEREMIAH

WIKI YA WAZEE

* Kwanini sherehe za jando na unyago hazifanyiki kama zamani?

* Wanawake wengi wanapendelea kuvaa suruali wakati wa safari hiyo inakuwaje maana si mavazi ya asili?

14th MAY 2022 RUTH SHABANI SUDI

WIKI YA WAZEE

* Kwanini mila na desturi mbaya kama vile ukeketaji kwa wasichana zilikuwa zinafanyika wakati zilikuwa na madhara katika jamii?

RICHARD · L · SIMON

WIKI YA WAZEE

14/5/2022

1) Je mlivyokuwa mnaishi kizamani na sasa, ~~sat~~ staili ya sasa tunayoishi ndo inafaa kwasisi tunavyofikiri vijana kwani kuna matatiz tuliyo yasikiya enzi ya nyuma kama, @ ukeketaji kwa wasichana, je staili ya zamani inafaa kurudia kuishi?

II) Je ni mtu gani aliye anzisha hii michezo ya asili kama vile bao, tikri, mruko wa juu

14/05/2022

## WIKI YA WAZEE

(i) Kwanini makabila mengi yameanza kusahau mila na tamaduni zao

(ii) Kuna madhara gani kama tutaacha mila na desturi zetu ~~[illegible]~~

GERTRUDE-DANIEL

14/5/2022

# WIKI YA WAZEE

## Swali

- Kwa nini tamaduni za sasa na za kale zinatofautiana
- Kwa nini uvaaji wa vijana wa sasa na wa kale uno tofauti
- Kwa nini ulaji wa vyakula vya asili vimepotea kwa kizazi cha sasa

WIKI YA WAZEE
SUZANA STEPHANO
MASWALI
14/05/2022

1. Chakula cha ~~wazee~~ asili kinafaida gani kwetu?
2. Kwanini hizi mila na desturi za zamani walikuwa wanaw
keketa wanawake?
3. Kwanini hizi mila za kimasai vijana wanatairiwa bila ga
mi na wanatairiwa wakiwa vijana wakubwa na so wadogo
4. Kwanini wamasai ~~ka~~ hawavazagi nguo bali wanajifunika mashuk
5. mnatushauri vipi vijana wa sasa juu ya mavazi tunayovaa?
6. JP? Nikwanini wazee wa zamani walikuwa wanafanya vikao vyao
chini ya mti/miti?

14-5-2022

# WIKI YA WAZEE

- Ni vyakula gani mngewazasi. Vijana mtushauri tutumi